# USHIRIKISHWAJI WA JINSIA NA VIJANA KATIKA USHIRIKA

**SULEMAN A. CHAMBO**

**MHADHIRI CHUO KIKUU KISHIRIKI CHA**
**USHIRIKA NA BIASHARA MOSHI**

**MADA ILIYOTOLEWA KWENYE KONGAMANO**
**LA UZINDUZI WA MWAKA WA UMOJA WA**
**MATAIFA WA USHIRIKA**

**DAR ES SALAAM, 21-22 MACHI, 2012**

## 1.0 UTANGULIZI

Taasisi ya ushirika ina umri wa miaka 168, tangu ilipoibuliwa huko Rochdale Uingereza. Ushirika huu si sawa sana na ule wa jadi, ulioishi barani Afrika kwa muda mrefu huko nyuma, ingawa baadhi ya maudhui yanakaribiana.Dhana ya ushirika wa jadi, na şuala la watu kushirikiana halikuwa na mjadala kwa sababu lilikuwa ni tendo la kanuni za jadi na lililenga kuihifadhi jamii ili iendelee kuishi kwa vile kushirikiana kulikuwa ni sehemu ya maisha ya uchumi wa kujikimu ambao ulikuwa hauzalishi ziada. Ushirika huu ulilazimika na bila kufanya hivyo, jamii ilikuwa hatarini kupotea kwa kukosa usalama wa chakula. Watafiti kama Craig, 1976, wameuita ushirika moja kwa moja au (automatic co-operation) au ushirikajadi.

Ushirika tunaozungumzia leo, ni ule ambao watafiti wameuita ushirika mkataba Ushirika huu , una chimbuko la kujibu matatizo ya kuibuka kwa mapinduzi ya uchumi wa viwanda huko Ulaya , hususan Uingereza. Kwa mantiki yake, ushirika mkataba, ni ule amabao watu hujiunga kwa hiari na uhuru wao ili kuunda taasisi ambayo wanachama wanaipa majukumu ya kukidhi mahitaji yao ya kiuchumi na kijamii. Asasi hii inaundwa na wanachama ili waitawale na waiendeshe kwa misingi ya demokrasia.

Ushirika mkataba **(contractual co.operation)** ulianza hapa Tanzania takriban miaka 80 iliyopita na ushirika huo ndio unaotambuliwa na Umoja wa Mataifa amabao uzinduzi wake ulifanywa jana. Hata hivyo ikumbukwe kuwa ushirika tunaozungumzia hivi leo, umepitia awamu nne za mabadiliko ya sera za uchumi na hivi leo tunaweza kusema ushirika bado unaendelea kujijenga ndani ya tamaduni za uzalishaji mali za nchi yetu. Mazingira ya ushirika ulipoanza huko Uingereza, yalikuwa ya mfumo wa ubepari wa viwanda. Wakati ulipoanzishwa hapa kwetu mfumo wa kiuchumi ulikuwa ule wa wakulima wadogo. Utamaduni na shughuli za taasisi hii vilikuwa tofauti nailipoletwa hapa kwetu. Shughuli za ushirika kule ulikoanzia zilikuwa maduka ya walaji na hapa kwetu ushirika ulianzia na mazao ya biashara ya wakulima wadogo wadogo. Pamoja na kwamba ushirika wa walaji ulianzishwa hapa kwetu, lakini haukuwa na nguvu kama ule wa mazao ya biashara. Hoja ya msingi hapa ni kuwa ushirika kama asasi ya kigeni ilihitaji muda wa kutosha ili iweze kukubalika katika uchumi wa kujikimu unaozalisha mazao ya biashara ambayo hapa Tanzania hayana soko hadi leo. Pili, mifumo ya utawala na demokrasia hapa kwetu, bado

haijatengemaa na kukubalika katika utekelezaji, tatu utekelezaji wa baadhi ya sheria hapa kw vile vile hapa kwetu, bado ni hafifu kiasi kwamba uwajibikaji unaonekana ni vigumu kutekelezeka. Haya yote ni mambo ya kutilia maanani tunapouchambua ushirika mkataba katika mazingira ya Tanzania na Afrika kwa ujumla wake.

Nataka nibaini mambo mawili hapa kuwa ushirika Tanzania ulianza na mazao ambayo hayakuwa na uhitaji hapa kwetu. Pili kwa miaka yote hiyo hadi leo, hatujawa na ushirika wenye soko la ndani ya nchi yetu. Ingawa ushirika wa mazao ya chakula ulianzishwa, lakini haukuwa na nguvu kwa vile pengine ulikuwa hauleti fedha za kigeni. Mkanganyiko wa kuzalisha mazao ya biashara ambayo hayana soko la ndani. Hali hii naiita janga la kihistoria (historical tragedy) kwa sababu nguvu ya ushirika wa mazao ya biashara haikua mikononi mwetu bali uko nchi za kigeni.

Katika mada hii tutazungumzia masuala muhimu ya ushirikishaji jinsia na vijana kwa kuzingatia mambo yafuatayo:- Kwanza tutaangalia uchambuzi wa tatizo a ushiriki wa jinsia na vijana katika ushirika. Pili tutachambua nadharia ya ushirikishwaji wa jinsia na vijana katika ushirika. Pili tutafanya .uchambuzi wa tatizo la ushiriki wa jinsia na vijana katika. Tatu tutafanya uchambuzi wa hali halisi ya ushirika hapa kwetu Tanzania ili kuliona tatizo la ushirika kwa uwazi zaidi hasa kweye upande wa ushirikishwaji wa jinsia na vijana. Napenda niliweke wazi suala hili kuwa hapa hatuna nia ya kumlaumu mtu ye yote au kutafuta mchawi, bali tunataka kuzungumzia hali ilivyo leo ili sisi wote tujipange upya kuujenga ushirika. Mwisho, tutatoa mapendekezo ya kimkakati na kimfumo ili tuweze kuchangia katika mstakabali mpya wa ushirika unaoshirikisha jinsia na vijana.

## 2.0 UCHAMBUZI WA TATIZO LA USHIRIKISHWAJI WA JINSIA NA VIJANA KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA TANZANIA

Nchini Tanzania, tunaipongeza serikali kwa kujenga mihimili muhimu sana ya miundo mbinu ya kitaasisi ili kuunga mkono juhudi za maendeleo ya ushirika nchini. Miundo mbinu ya kitaasisi ni pamoja na kuwepo kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara. Chuo hiki kilijengwa kwa makusudi ya kutoa elimu ya ushirika kwa wanachama , viongozi na watendaji wao. Chuo kina muundo mfiko unaosambaa nchi nzima kupitia mikoani. Kwa muundo mfiko huu tunatarajia kuwa wanachama wanawake na wanaume watafikiwa na elimu ya ushirika wakiwa mikoani kwao. Tuna shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika

(COASCO). Shirika hili linafanya kazi kubwa ya ukaguzi wa vyama vya ushirika mikoa yote ya Tanzania bara. Kikubwa hapa ni kuwa Tanzania ina shirika la ukaguzi ambalo linatoa huduma za kujenga nidhamu, haki na demokrasia kwa gharama nafuu. Tatu tuna Idara ya serikali inayofanya qudhibiti na ukaguzi wa ndani ikishirikiana na Kamati za ukaguzi ndani ya vyama vya ushirika ili haki itendeke na kujenga misingi ya utawala bora katika vyama vya ushirika. Nne tuna sera ya ushirika ya mwaka 2003 ambayo rasmi inatambua uwepo wa makundi yaliyo pembezoni kama wanawake, vijana na watu wenye ulemavu (URT:2003). Kuna sheria ya Ushirika inayojaribu kutekeleza maudhui ya sera ya ushirika pamoja na kanuni zake. Kwa upande mwingine sheria imeruhusu uundwaji wa vyama vya ushirika ikitambua ngazi mbili zile za vyama vya msingi na ile ya shirikisho kwa kutoa nafasi ya kuunda ngazi ye yote ya kati kwa angalizo kuwa miundo yo yote ile inayoundwa , izingatie gharama na kufanya maamuzi ya haraka katika kufanya biashara ya ushirika.

Aidha katika nchi za Afrika kusini mwa Jangwa la Sahara, hakuna nchi yenye miundo mbinu ya kitaasisi katika kuhudumia ushirika kama Tanzania. Pamoja na juhudi Zote za ujenzi wa miundo mbinu ya kitaasisi na kuwa na sera na sheria zinazotekelezeka, serikali ya Tanzania imekwenda hatua ya juu zaidi kuandaa mpango Kabambe wa maboresho na modanizesheni ya vyama vya ushirika ili utekelezaji wa sera na sheria vitekelezeke kwa uwazi zaidi.

Haya yote yakifanyika kwa upande wa serikali na taasisi zake, bado tunashuhudia tatizo kubwa la ushiriki hasi wa jinsia na vijana katika ushirika. Je tatizo liko wapi au kulikoni.? Katika mada hii tunataka kujenga hoja kuwa ushirika wenyewe haujajiangalia ndani ili kubaini vikwazo vya ndani ya ushirika ambavyo vinakwamisha ushiriki wa jinsia na vijana katika ushirika nchini Tanzania. Vikwazo hivyo, viko katika maeneo manne. Kwanza ni ushirika ambao haupanuki kwa kasi kisekta, kiaina na kishughuli, ili kutoa fursa ya ushiriki wa watu mbali mbali uliopanuka kwenye nyanja nyingi amabako ushirika ungeweza kuanzishwa. Eneo la pili la tatizo ni uwekezaji hasi katika maisha ya sasa na ya baadaye ya wanachama wa vyama vya ushirika. Tatu ni uwezo hasi wa kutumia fursa zilizotolewa na serikali kuwaandaa wanachama kuzishabikia fursa hizo ki ushirika na nne ni kuendelea na teknolojia ya uchumi wa kujikimu ambayo inabadilika pole pole sana.Tano, ni Picha hasi ya ushirika ndani ya jamii. Haya ni maeneo ambayo yanasheheni tatizo kuu la kuwa na ushiriki hasi wa jinsia na vijana katika ushirika . Maeneq haya yakifanyiwa kazi, ushirika wetu utaanza kufanya kazi yake kubwa ya kuongeza wanachama wake. Kabla hatujaingia katika

hali halisi ya matatizo ya ushiriki wa jinsia na vijana kwanza tupitie kwa ufupi nadharia za ushirika shirikishi katika ushirika, jinsia na vijana.

## 3.0 NADHARIA YA USHIRIKI SHIRIKISHI, JINSIA NA VIJANA

### 3.1 Binadamu na Uchumi Vikundi

Nadharia ya ushirikishwaji, inamwangalia binadamu akiwa peke yake na akiwa mmoja wa wanakikundi. Maisha ya kiuchumi ya binadamu akiwa peke yake, yamebeba upungufu mkubwa ambao unamweka binadamu huyo katika mazingira hatarishi. Mwandishi mmoja wa masuala ya umasikini (Chambers :1996) ameeleza kuwa umasikini ni hali hatarishi ambayo binadamu anajikuta hana uwezo wa kutawala maisha yake na mifumo inayomzunguuka inaendelea kumnyang'anya mali akibaki hana kitu wakati wote. Aina moja ya mifumo inayomnyang'anya mali zake , ni pamoja na mfumo wa soko huria. Kwahiyo binadamu huyu, akiingia kwenye kikundi, anapata fursa na mbinu za kupambana na mifumo inayomnyang'anya mali ili aondokane na umaskini. Akiwa katika vikundi, anaweza akaingia sokoni akapata nguvu za kupewa bei nzuri ya mazao yake,akazalisha kwa gharama ndogo,akapata madaraka ya kuamua kuhusu malengo yake ya baadaye ya kiuchumi . Kwa mantiki hii ya uchumi vikundi, binadamu anapata ukombozi wa kukuza uzalishaji wa mazao na huduma ili aondokane na maisha yenye mazingira hatarishi na umasikini. Haya ni matokeo ya binadamu kushiriki katika uchumi vikundi. Lakini je ushiriki na ushirikishwaji ni nini?

### 3.2 Ushiriki na Ushirikishwaji

Ushiriki na ushirikishwaji ni mchakato wa kuwapa wananchi walio wengi na maskini, fursa ya kutambuliwa kuwa nao wana madaraka ya kijamii na kisheria kudhibiti na kufanya maamuzi kuhusu uzalishaji na udhibiti wa mgawanyo wa mali kwa faida yao na taifa zima.(Narayan: 2000). Kuwatambua maskini na wazalishaji wadogo na kuwashirikisha kunahitaji mambo makubwa yafuatayo:

i) Ni muhimu kubadilisha sheria na kanuni za utambuzi wao wa haki ,taratibu na michakato itakayowapa uwezo wa kisheria kujadili mambo yanayowasibu kwa uwazi, na kuchukua hatua muafaka ili kuleta mabadiliko waliyopanga na kuyafikia. Ushirikishwaji haushii kwenye tamko tu, bali ni lazima utekelezwe kivitendo na wahusika wayaone matokeo yake na kuyapima.Kila mara tunakuwa na mabadiliko ya sheria za ushirika . Nia ni kuwatanbua wanaushirika ili washinki kikamilifu. Katika ushirika.

ii) Pili, ilin ushiriki wa watu uwe na tija,wanaoshiriki ni lazima wawe na mfiko wa taarifa muhimu zinazohusu uchumi wao Hii ni pamop na kupata taarifa za bei za mazao, masoko yaliko wanunuzi wa mazao yao na aina ya usafirishaji wa mazao yao.Serikali na hasa dola linatakiwa liwape taarifa muhimu wananchi wake hasa wale wanyonge ili watumie taarifa hizo kwa maamuzi na kuandaa mikakati ya kujikomboa kutoka umaskini.

iii) Tatu ni uwajibikaji wa dola na vyombo vingine vya utawala kwa wananchi wake. Mjadala kuhusu ushiriki na ushirikishwaji unajenga ujasiri ndani ya wananchi na unakamilika pale ambapo viongozi waliopewa madaraka ya kutawala, wanaona umuhimu wa kuwajibika kwa matendo yao (Narayan :2000) anazungumzia kuwa viongozi wa serikali au taasisi kama vyama vya ushirika wanatakiwa kuwajibika pindi inapodhihirika kuwa wanahusika na madhara yo yote ya unyang'anyi wa mali za wanachama,

### 3.3 Ushiriki wa Jinsia

Tunapoangalia suala la ushiriki wa jinsia katika ushirika tunazungumzia fursa za haki sawa kwa wanaume na wanawake kushiriki katika uchumi vikundi ili waondokane ma maisha hatarishi na umaskini. Hoja ya msingi hapa ni kuwa wanawake hawajapewa haki sawa ikilinganishwa na wenzao wanaume ili nao washiriki katika shughuli za ushirika nchini. Kwa upande wa ushiriki wa jinsia katika ushirika, nadharia inasema jinsia ya kike haijapewa fursa sawa ya kushiriki katika ushirika kwa sababu jamii yetu bado inatawaliwa na mfumo dume. Katika mfumo huo, kuna majukumu matatu ambayo yanamwengua mwanamke kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za ushirika kama ifuatavyo:

#### 3.1.1 Uzazi na Uondclczaji wa Familia

Katika jamii yetu, wanawake wamepewa kazi za uzazi na uendelezaji wa nyumba na familia. Kazi hizi hufanywa ndani ya nyumba, nazo ni kuzaa watoto, kupika, kufua nguo,kutafuta mboga na kuni.Ukiacha kuzaa ambayo inatokana na hali halisi ya kuwa mwanamke, kazi nyingine zote za ndani ya nyumba , zinaweza kufanywa na jisia ya kiume. Hata hivyo kuna mambo matatu ya kuzingatia katika hili; Kwanza kazi hizi hazijatambuliwa na jamii wala taarifa za takwimu za uzalishaji. Pili kazi hizi hazilipwi ujira wo wote na tatu, hizi ni kazi ambazo zinachukua muda mwingi wa wanawake , na hivyo kuwapa kipingamizi cha kushiriki kazi za nje ya nyumba kama kuwa wanachama kwenye vyama vya ushirika . Takwimu za kiutafiti zinaonyesha kuwa wanawake wa Tanzania wanafanya kazi za ndani

kwa saa 16 hadi 18 kwa siku na wenzao wa jinsia ya kiume wanafanya kazi za Uzalishaji Mali kwa saa 8-10 kwa siku.

### 3.1.2 Kazi za Uzalishaji Mali na Huduma

Hízi ni kazi za kuzalisha mali na huduma kwa ajili ya kujikimu kiuchumi katika familia. Hapa vile vile kuna mgawanyiko ambao unawanyima wanawake fursa ya ya kushiriki katika ushirika. Hapa imejidhihirisha kuwa kazi za kuzalisha mazao ya biashra na yenye mapato makubwa kweye ushirika kama kahawa, tumbaku na korosho, zinasimamiwa na wanaume pamoja na mapato yake, na kazi za kuzalisha mazao ya chakula zaidi zinafanywa na kusimamiwa na wanawake. Wanawake wanachangia nguvu kazi kwenye uzalishaji wa mazao ya kwao nay a wanaume, Lakini kwa vile mazao ya wanawake hayatambuliwi kwenye biashara ya ushirika mwanamke anakuwa kaenguliwa kuonyesha ushiriki wake kwenye ushirika wa mazao ya kilimo.

### 3.1.3 Kazi za Jumuiya Nje ya Nyumba

Kuna kazi za jumuiya ambazo watu wanashiriki nje ya familia ambazo mara nyingi ni za kujitolea kama uongozi wa vikundi vya jamii, kujtolea ujenzi wa shule na barabara. Kazi hizi zinafanywa na jinsia zote na zinachukua muda na mali. Lakini kwa vile mwanamke ana majukumu mengi tayari, anaonekana ana muda mfupi sana wa hali, muda na mali kuweza kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za ushirika.

### 3.2 Ushiriki wa Vijana

Katika jamii zetu, kijana wa kike au wa kiume hajawa mtu mzima kisheria kabla hajafikisha umri wa miaka 18. Lakini kwa maana ya kuwa mtu mzima , kama hajaoa au kuolewa, bado ni mtoto mdogo. Kwa mantiki ya maainisho haya, vijana wengi ndani ya familia wanapata haki finyu kama walivyo wanawake. Ikiwa ni kuhodhi mali , ardhi au mazao ya biashara , vijana wanachangia nguvu kazi, lakini hawana fursa kubwa ya kushiriki katika mgao wa matokeo ya kazi za ushirika. Kwa maainisho ya umri na hali ya kuoa na kuolewa, inajidhihirisha kuwa itachukua muda mrefu sana kwa vijana kujiunga na vyama vya ushirika kwa sababu kwa muda mrefu ni watu tegemezi , hawana ardhi na hawana mali nyingine hadi hapo baadaye. Hali hii imekuwa kikwazo kikubwa kwa ushiriki wa vijana kwenye ushirika.

## 4.0 HALI YA USHIRIKA TANZANIA NA VIKWAZO VYA USHIRIKI WA JINSIA NA VIJANA

Kama tulivyosema hapo awali, ushiriki wa jinsia na vijana katika ushirika, una vikwazo kadhha ambazo kama havikutiliwa maanani, ushirika wetu utaendelea kuwa wa mfumo dume na wanachama wazee. Mambo tuliyozungumza kuwa yanauvuta nyuma ushirika wa Tanzania, kama ifuatavyo:-

### 4.1 Ushirika Usiokua na Usiopanuka

Wote tumeshuhudia athari za şoko huru na jinsi lilivyoanzishwa bila maandalizi. şoko hiti liliathiri sana kukua kwa ushirika. Pamoja na hayo, mwaka 1997, Shirikisho la vyama vya Ushirika wakishirikiana na serikali, waliitisha mkutano mkubwa sana wa wadau wa ushirika uliohudhuriwa na wajumbe kutoka taasisi zote amabazo zina shiriki katika maendeleo ya ushirika. Mapendekezo mahsusi ya kuupanua na kuuandaa ushirika kwa ushindani yalitolewa. Kwa bahati mbaya ripoti ilikwama mahali na haikutoka hadi leo. Ukiangalia takwimu za idadi ya vyama vya ushirika za hivi karibuni, utaona kuwa idadi ya vyama vya ushirika iko kwenye mdororo mkubwa kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali Na 1 hapa chini.

**Jedwali i: Idadi ya Vyama vya Ushirika kama iliwokuwa Machi 2011**

| Aina ya ushirika | Asilimia ya idadi iliyopo% |
|---|---|
| Akiba na Mikopo | 55.3 |
| Ushirika wa Kuuza Mazao ya Biashsra | 29.6 |
| Ushirika wa Huduma | 3.1 |
| Ushirika wa Viwanda | 2.0 |
| Ushirika wa Mifugo | 1.2 |
| Ushirika wa Uvuvi | 1.3 |
| Ushirika wa umwgiliaji | 1.1 |
| Maduka ya ushirika ya walaji | 1.1 |
| Ushirika wa Madini | 0.6 |
| Ushirika wa Nyumba | 0.3 |
| Usafirishaji | 0.04 |
| Vinginevyo | 2.8 |
| Kilele | 0.02 |
| Vikundi | 0.8 |

**Chanzo**: Idara ya Maendeleo ya Ushirika Dodoma

Dhana ya ushiriki wa makundi ya watu kama wanawake na vijana katika ushirika inabeba mambo makubwa mavvl!i ambayo si lazima yaende sanjari; Kwanza ushinki ni tendo la kuwa mwanachama kwa kununua hisa ili mtu awe mwanachama kamili. Hii mara nyingi ni rahisi kutekeleza hasa kama wanachama wana elimu ya kutosha kuhusu ushinka wanaojiunga nao. Jambo la pili ni ushiriki wa mwanachama katika uzalishaji utumiaji wa huduma za ushinka na kushiriki katika kuchangia maamuzi ya kibiashara ya kusimamia na kudhibitl mwenendo wa ushirika wake.

Sura inayojitokeza katika takwimu zilizotolewa, ni kuwa ushirika uko katika sekta chache sana na ni mfinyu kishughuli. Katika ushirika mfinyu kama inavyoonekana, itakuwa vigumu sana kwa makundi ya wanawake na vijana kushiriki kama wanahisa na washiriki katika mijadala ya kuleta maendeleo ya ushirika nchini. Sekta ya huduma za fedha ni ushirika unaokua kwa haraka, lakini bado uko ngazi ya msingi na haujafika ngazi ya sekondari maana ya uanzishwaji wa benki za ushirika za mikoa , isipokuwa Kilimanjaro na Kagera.

Kwa upande wa mazao ya biashara ya kilmo, kuna matatizo ya aina mbili kubwa; Kwanza mabadiliko makubwa hayajafanyika kuhoji utendaji kazi wa vyama vikuu katika mfumo wa soko huru. Sheria mpya ya ushirika ya mwaka 2003, inazungumzia umuhimu wa ngazi mbiti, yaani msingi na kittaifa na kama kuna ngazi yo yote kati ya hizo , basi itokane na uchambuzi wa gharama na wanachama ili muundo muafaka unaokwenda na matakwa ya wanachama uibuliwe. Hili halijafanyika na linazuia ushiriki wa jinsia na vjana katika ushirika kwa vile uchambuzi wa kina ungebaini namna ya kutekeleza maudhui yaliyopendetezwa na sera ya ushirika ya mwaka 2003. Tatizo la pili ni ushirika wa mazao kutopanuka kishughuli ili kuongeza thamani ya mazao yanayozalishwa na wanachama. Ushirika wa pamba, kahawa na korosho ulianza vizuri kwa kuwa na ngazi za usindikaji ili kuongeza thamani. Lakini ngazi hizo zimekuwa zikiptgwa vita na taasisi za mashinka binafsi ili vyama vya ushirika vibaki pembezoni. Ushinka wetu wa mazao umebaki wachuuzl wa malighafi na kutokuingia ngazi ya usindikaji, kunaufanya ushirika huu usiruhusu wanawake wengi na vijana kujiunga nao.

**4.1 Uwekezaji Hasi**

Mali nyingi ambazo vyama vingi vya ushirika sasa hivi zipo ni zile zilizojengwa miaka ya 1950-60. Majengo, mitambo, vyombo vya usafiri , mashamba ya mfano, viwanda vinatokana

na uwekezaji uliofanyika miaka ya nyuma. Shirikisho Ia vyama vya Ushirika, hivi sasa limeanzisha dhana ya uwekekezaji na kuboresha kitega uchumi kilichozinduliwa miaka ya 1960. Hatua hii inawaonyesha wanachama, kuwa ushirika unahitaji kujenga vitega uchumi ambavyo vitaboresha maisha ya wanachama sasa na hapo baadaye.

Hata hivyo kuna mambo matatu ambayo wanachama wa vyama vya ushirika wanatakiwa kuyabaini ili uwekezaji uzingatie ushiriki wa wanawake na vijana nayo ni kama yafuatayo; Kwanza kuwekeza katika teknolojia zinazopunguza kazi za mikono ndani ya familia na uzalishaji shambani na kuhimiza usindikaji ili maeneo ya ushiriki wa wanawake na vijana yaongezeke, Pili sehemku kubwa ya mgao wa zidio uelekezwe zaidi kwenye uwekezaji ili kuongeza uzalishaji na kuwaimarisha wanachama katika uzalishaji na tija pamoja na ushiriki mpana wa wanawake na vijana.

Suala Ia tatu ni mabadiliko yanayoashiria kupanuka kwa shughuli za fedha katika ushirika ambazo zinajenga na kuhifadhi maisha ya wanachama wa ushirika. Tunasisitiza kuwa uundwaji wa benki za ushirika kiwilaya , kimkoa, kitaifa na ki kanda utaimarisha uwekezaji ndani ya ushirika kukamilika kwa kubakiza zidio Ia biashara katika mfumo wa kifedha wa ushirika. La pili katika ushirika ni kuwa, hivi sasa, maisha ya wanaushirika bado yako kwenye mazingira hatarishi . Mtu anaweza kuwa mwanachama wa chama cha ushirika kwa miaka hamsini ya maisha yake. Lakini kwa vile siku anastaafu kuwa mwanachama, anarudishiwa hisa zake na kama hisa hizo zilikuwa na thamani ya shillingi 5,000, basi mwanachama huyu mzee anarudishiwa shillingi zake 5,000 na anakwenda zake nyumbani. Hii haiwahakikishii wanachama usalama wa maisha ya baadaye baada ya kustaafu kwenye ushirika. Ni vizuri ushirika sasa ukaangalia kuwa na vyama vya ushirika wa bima ili mwanachama aweze kuwekkeza kwenye bima za ushirika na mifuko ya pensheni ya ushirika ili kuwahakikishia ubora wa Maisha wanaushirika sasa na hapo baadaye. Ni rahisi kumkata mwanachama wa chama cha kuuza mazao shillingi 200 kila kilo ili awekeze kwenye mfuko wa pensheni yake atakapostaafu. Kutokuwa na uwekezaji wa namna hii kunawakatisha tamaa makundi ya wanawake na vjana wasijiunge na vyama vya ushirika.

### 4.2 Uwezo Hasi wa Kutumia Fursa Zilizopo

Vyama vya ushirika vilivyopo vina changamoto ya kutotumia vema fursa zilizotolewa na sera ya ushirika na taasisi zilizopo zinazosaidia maendeleo ya ushirika. Tukiangalia

maudhui ya sera ya ushirika ya mwaka 2003, tunaona fursa zifuatazo ambazo bado hazijatumiwa na vyama vya ushirika kwa ukamilifu zaidi. Sera ya ushirika inazungumzia wazi wazi kuwa serikali itahakikisha kuwa wanawake wanashiriki kikamilifu katika shughuli za ushirika , kuwahamasisha wanawake kuwa wanachama wa vyama vya ushirika na kuwahamasisha kuchukua nafasi za uongozi. Vile vile serikali iliazimia kuwapa wanawake upendeleo maalum katika kupata elimu na mafunzo. Serikali itayapa msukumo makundi mengine ya jamii ambayo yako pembezoni kama vijana na makundi ya watu wenye ulemavu. Miaka ya 1995-1999 nikiwa kiongozi wa Chuo cha Ushirika nilimuelekeza Mrajis wa Mafunzo wa Chuo kuangalia ambavyo tungeweza kushusha ada kutoka laki saba za wakati huo hadi laki tano ili iwe rahisi kwa vyama vya ushirika kushiriki katika mafunzo. Tulipotangazia vyama vya ushirika kuhusu unafuu huo tulipata majibu kutoka vyama viwili tu, nasi tulitaka darasa la wanafunzi 40 kwa kuanza.

Serikali vile vile iliazimia kuviwekea vyama vya ushirika mzingira mazuri ya kuhimili ushindani na namna ya kuazisha vyama Vya ushirika katika sekta nyingi zaidi. Ili kuleta uwiano mzuri na uchumi wa ushindani serikali iliazimia kupunguza ngazi za ushirika kutoka nne za zamani hadi mbili. Pamoja na kwamba sera haikutiririsha masuala ya jinsia, lakini kilichoonekana ni vyama vya ushirika kutotimiza mambo mawili makubwa katika utekelezaji. Kwanza kutokuwa na mpango mkakati wa kuleta mabadiliko makubwa ndani ya UShirika. Katka mpango huo wa mabadiliko makubwa, maeneo ambayo yanatoa fursa kupitia sera yangeainishwa vizuri na kuunda timu ya kikosi kazi cha wanachama kwenda kukutana na serikali kuhusu namna bora ya kutekeleza maudhui na fursa zilizotamkwa na serikali katika sera.

Mchakato huu ungelibaini maeneo muhimu sana ya ushiriki wa jinsia na vijana kwa ukamilifu zaidi. Kwa upande wa vijana, vile vile tunaona kuwa serikali ya Tanzania ina sera ya maendeleo ya vijana, lakini ushirika katika ngazi zote, haujalifanyia kazi suala la kuwa

na mkakati na programu maalum ya kuwashirikisha Vijana katika ushirika. Lakini ukweli unabaki pale pale kuwa katika nchi nyingi za kiafrika na Tanzania ikiwa mojawapo, kundi la vijana ni kubwa kwa asilimi kuanzia 50% hadi 70% ya idadi ya wananchi wote. (Chambo na wengine:2007). Pamoja na kwamba sera ya ushirika ya 2002, ilitamka wazi wazi mahitaji ya kuanzishwa kwa elimu ya ushirika shuleni, mpaka sasa tuna changamoto ya kuingiza

elimu ya ushirika kama sehemu ya elimu ya ujasiriamali ili vijana wengi wajifunze ushirika ili tuanze kuwajenga wanaushirika wa kesho tukianzia shuleni. Tamko hili halijafanyiwa kazi ingawa mwaka 1995, baada ya Shirika la Kazi Duniani kutoa fursa ya kuwasiliana na Wizara zenye dhamana ya elimu ili tuone kama inawezekana kuanzisha mitaala ya elimu ya ushirika shulenina vyuoni. Kazi ya awali tuliifanya na jibu tulilopata kutoka Wizara ya Elimu wakati huo, ni kuwa mitaala ya shule ilikuwa imejaa, Lakini tulipojadiliana na VETA, ilijidhihirisha kuwa walikuwa na uhitaji mkubwa wa kuwekeza katika elimu namafunzo ya ushirika kama sehemu ya ujasiriamali katika elimu ya ufundi nchini. Wazo hili bado halijafanyiwa kazi lakini sasa linawezekana na hili likifanyika , ushirika utakuwa ni taaluma muhimu katika elimu ya ufundi na itaanza kuwaunganisha vijana katika ushirika nchini.

### 4.4 Teknolojia ya Uchumi wa Kujikimu

Ushirika ulipoanzishwa huko Uingereza mwaka 1844, ulitokana na uchumi wa Viwanda unaozalisha ziada ambayo ni lazima itafute soko po pote lilipo. Pamoja na kuwa aina ya ushirika ulipoanza ulikuwa ushirika wa walaji wa mazao ya VlWandani na yale ya kilimo, cha msingi ni kuwa ulianza katika mazingira ya ya teknolojia iliyokuwa inaashiria uzalishaji wa hali ya juu wa ziada. Ushirika ulipoingia hapa kwetu, ulianza na wakulima wadogo wadogo waliokuwa wanatumia teknolojia Ya hali na hadhi ya Chini. Teknoloji hiyo ilikuwa inazalisha ziada ndogo sana lakini kwa Vile bidhaa zilizozalishwa kwa uhakika hazikuhitajika hapa kwetu, ushirika ulionekana kushamiri kwa kasi.

Pamoja na kushamiri huko, ushirika haukujiigiza katika mabadiliko makubwa ya teknolojia ya uzalishaji wa ziada kubwa. Sababu za kutobadilisha mifumo ya teknolojia za uzalishaji hazifahamiki sana lakini kulikuwa na mikanganyiko ya aina mbili. Kwanza ni fikra kuwa wakulima wadogo ni maskini na hata wakiwa wanachama wa vyama vya ushirika hawatabadilika sana maana vyama vya ushirika ni vyombo vya wanyonge. Kwa dhana hii inakuwa vigumu kufikiria kuwa mwanachama mkulima anaweza kubadilisha teknolojia ya uzalishaji ikawa bora zaidi na akaondoka katika unyonge Wake. Tatizo la pili ni tulipoingia katika sera za ujamaa na kujitegemea ambapo teknolojia inayoboresha uzalishaji ilihusishwa na ubepari. Na teknolojia duni ya zamani na inayomkwamisha mkulima ilioneka ndiyo ya kijamaa.

Dhana hizi mbili zilidhoofisha ushirika na zilikuwa kizingiti kikubwa kwa kuleta usawa wa jinsia na Vijana kwa sababu mbili kubwa. Kwanza uduni wa teknolojia haukulta mabadiliko makubwa yanayohitaji nguvu kazi kubwa ambayo ingewaalika wanawake na vijana kuwa wanashama na washiriki wakubwa wa ushirika . Pili teknolojia duni inapohusihwa na vyama vya ushirika , haina mvuto kwa jamii , hususan vijana. Tamko la Kilimo Kwanza linaweka bayana kuwa kilimo kinahitaji mabadiliko makubwa ya kiteknolojia katika uzalishaji na usindikaji. Hata hivyo,, sekta ya UShirika katika ujumla wake haijalifanyia kazi tamko hili. Badala yake inawezekana wengi tunalalamika kuwa tamko la Kilimo Kwanza halijatamka ushiriki wa vyama Vya ushirika kwenye mkakati wa Kilimo Kwanza. Kutotamka ushiriki wa ushirika kisiwe kikwazo kwa ushirika , hasa shirikisho, kuamka na kutafuta majibu kutoka serikali kuu katika utaratibu wa mijadala shirikishi ya pamoja.

### 4.5 Plicha Hasi ya Ushirika Ndani ya Jamii

Mara nyingi, Wama vyama vya ushirika vinaongozwa na misingi ya uwazi, demokrasia na uwajibikaji. Wakati wa mikutano mikuu, viongozi wanatoa taarifa za mafanikio na changamoto za ushirika wao. Mara nyingi vyombo vya habari vinatangaza Changamoto kama za ubadhirifu, rushwa na mambo yanayofanana na hayo. Kwa jamii iliyoko nje ya ushirika , Picha wayopata ni ya kukatisha tama kuwa kwenye ushirika kumejaa ubadhirifu tu na hakuna mema., Hii imezuia watu wengi kutokushiriki shughuli za ushirika ikiwa ni pamoja na wanawake na vijana.

## 5.0 MABADILIKO YA USHIRIKA NA TAASISI KATIKA KUPANUA USHIRIKI WA JISIA NA VIJANA

Miaka hamsini ya Uhuru imepita pamoja na misukosuko mingi katika siasa, sera na uchumi, ushirika bado upo na ni ni taasisi inayotegemewa na wengi. Pili tuna mfumo wa kitaasisi ambao unaweza ukafanyiwa kazi ukaanza kuleta mabadiliko makubwa kwa wanachama na hususan ushiriki wa jinsia na vijana. Yafuatayo ni mapendekezo ya mikakati na mbinu za kuleta maboresho na mabadiliko katika ushirika na taasisi zake ili kuongeza ushiriki wa jinsia na maendeleo ya ushirika mpya nchini Tanzania:

## 5.1 Kuandaa Mkakati wa Kuleta Mabadiliko Ndani ya Ushirika Wenyewe

Maendeleo ya ushirika yanatokana na mkakati wa majidiliano kati ya wadau wanaohusika na ushirika. Ni vizuri sasa Shirikisho la Vyama vya Ushirika likaandaa mkakati kabambe wa kufanya yafuatayo: -

- **Kufanya uchambuzi wa mahitaji ya ushirika katika sekta zote** ambazo kuna vyama vya ushirika lakini ni hafifu. Maeneo hayo ni kama uvuvi, ujenzi wa nyumba, usafirishaji, ushirika wa viwanda,umwagiliaji,madini, maduka ya ushirika na vikundi vingine. Uchambuzi huu utabaini uwepo wa mahitaji ya msingi ya kiorganizesheni ambayo kwayo, uhamasishaji wa namna ya kuanzisha vyama vya ushirika kwa misingi ya uwazi, deokrasia na uwajibikaji unaweza kuanza kwa kutumia utaratibu wa elimu ya uhamasishaji ambayo shirikisho linaweza kuifanya kwa kushirikiana na Tassisi ya Elimu ya Ushirika na Maendeleo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara.

- **Kuanzisha Kitonco cha Uchambuzi wa sora na Ufuatiliaji**
  Shirikisho la vyama vya Ushirika (TFC) ndicho chombo halali cha kuhamasiha ushirika nchini Tanzania. Tumeona kuwa maazimio mengi yanatolewa katika sera na sheria na programu mbali mbali za serikali na vyombo vingine. Lakini tunaona yanabaki matamko tu bila uchambuzi wa kina na kuandaa programu za muda mfupi mfupi. Programu hizo zitakuwa na agenda za kuwashirikisha wgnawake na vijana.
- Kufanya uchambuzi wa kina wa vyama vya ushirika uliopo na kuandaa hadidu za rejea kuhusu nguvu , upungufu , fursa na vitishio vya ushirika na maudhui yake ili kuona fursa ya kujenga mikakati ya ushirika uliofungamanishwa, na hasa kuangalia uwezo wao wa kuongeza wanachama hasa wanawake na vijana.

## 5.2 Mabadiliko ya Toknolojia

Kuna haja ya kufanya utafiti wa kina kuhusu uwezekanao wa kusindika mazao ili kuongeza thamani kwa mazao yote ili mazao yote yawe ya biashara. Kuna haja ya wizara ya Kilimo Chakula na Ushirika ikishirikiana na Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika na Biashara na Shirikisho la Vyama vya Ushiirika kuratibu utafiti wa kuibua

maeneo ya usindikaji wa mazao ambayo usindikaji ukianza , wanawake na vijana watapata fursa ya kushiriki katika ushirika endelevu.

### 5.3 Mfuko wa Elimu Wanaushirika.

Serikali ilianzisha Chuo Kikuu Cha Ushirika na Biashara kwa madhumuni makubwa ya kuendeleza elimu na mafunzo ya Ushirka kwa wanachama na viongozi na watumishi wa vyama vya ushirika Hii itaongeza ufanisi ili wału wa kawaida hasa wanawake na vijana wawe na imani na utendaji wa vyama vya ushirika. Wa nachama wapataomillioni moja , kama kila mwanachama atachangia kwenye mfuko wa elimu kusomesha wanaushirika sh 10,000 tutapata jumla ya shs tutapata billioni 10 kila mwaka ambazo ni guvu kubwa ya kusomesha mameneja 500 kwa mwaka na zinazobaki kuwaelimisha wanachama ili wausimamie ushirika wao vizuri na kwa ufanisi wa hali ya juu. Mpango wa mafunzo ujumuishe na mafunzo maalum ya ujasirishaji, ushirika na ujasiriamali.

### 5.4 Kuyajali Maisha ya Baadaye ya Wanachama

Siku ya uzinduzi Wa shereha za mwaka wa Ushirika Duniani, Rais Kikwete alisisitiza kuwa ushirika ni lazima uwavutie wanacham kuwa kama watajiunga nao kama wanachama, taasisi hiyo ionyeshe kuwa inawajali wanachama wake kwa maisha yao ya sasa na yale ya baadaye. Tumezungumzia kuwapo kwa benki ya ushirika na bima ya ushirika . Hizi ni taasisi ambazo kama zitajengwa na kuimarishwa, zitajenga mfumo wa kifedha ambao utasaidia kuvilinda vyama vya ushirika katika ushindani wa soko huru. Tasisi ya bima ya ushirika itakuwa inatoa bima mbali mbali kwa ajili ya vyama vya ushirika na kuiweka jamii ya wanaushirika kwenye maisha ambayo si hatarishi na endelevu. Taasisi za benki na bima za ushirika , zikipata faida, faida hiyo mwisho wake itarudi kwa wanaushirika wenyewe. Kukiwa na pensheni ya wanachama , hasa wakulima , kitakuwa kivutio kikubwa kwa wakulima, wafanyakazi na wanabiashara kujiunga na ushirika.

### 5.5 Mkakati wa Kuanzisha Elimu ya Ushirika katika shule , vyuo vikuu na vyuo vya Ufundi.

Vyama vya ushirika kwa kushirikiana na taasisi wadau wa maendeleo ya ushirika wawasiliane na kuratibu programu ya kuanzisha mafunzo ya elimu ya ushirika katika Shute za msingi, vyuo vya kati na vyuo vikuu kuendelea kujiandaa na kuwa wanaushirika wa baadaye.

5.6 Shirikisho liandae mkakati wa **utiririshaji wa masuala ya jinsia** katika vyama vya ushirika.

**6.0 HITIMISHO**

Katika mada hii tumejarinu kueleza mazingira ya ushiriki wa jinsia na vijana katika ushirika. Tumebaini sha kuwa pamoja na kuwa serikali imeandaa fursa nyingi kisera na mazingra mengine ya kuuweka ushirika kwenye mazingira ya ushindani, Vyama vya ushirika havija jiandaa kutumia fursa mbali mbali zinazotolewa ili kuwashirikisha wanawake na Vijana. Tumejaribu kueleza kwa nini wanawake na vijana hawashiriki kwa wingi katika ushirika na tukaona kuwa siyo fursa peke yake, bali kuna suala la teknolojia, uwekezaji wa sasa na baadaye na ushirika ambao haujapanuka kisekta kishughuli na kiteknolojia kama vikwazo vya msingi vinavyozuia wanawake na vijana washindwe kujiunga na vyama vya ushirika.. Mwisho tumeonyesha nini kifanyike kimkakati ili ushiriki wa jinsia na Vijana uonekane kwa vitendo katika mendeleo ya ushirika nchini

**REJEA**


Chambo, S, Mwani, M and 0100, O An Analysis of the Impact of Co-operatives in Poverty Alleviation and Their Institutional Context, ICA AND cca, Nairobi, 2006

Craig, J (1993) The Nature of Co-operation Black Rose Books, New York

Munkner, H, (2006) Co-operatives in Development Polic. *Journal of Cooperative and Rural Economics*, Vol 1. The Association for the Promotion of Cooperative Science and Rural Development Studies

Narayan, D (2000) Conceptual Frameworks and Methodological Challenges of Empowerments